# SHETANI TOA JAM

**Conrad Mghanga**




*All Rights Reserved. St. Francis Xavier Choir Mikindani-Msa*

# SHETANI TOA JAM



**SHETANI TOA JAM**



# SHETANI TOA JAM



# SHETANI TOA JAM




**SHETANI TOA JAM**

1. Pisha njia niende nikamuone Yesu- all-pisha njia shetani pisha pisha njia, nina kiu nataka nikamwone Mwokozi – all – pisha… S/A Nikamwone Yule (aliyeniokoa mimi) nikamwone yule (anaye nibariki mimi) nikamwone Bwana Mungu wangu (ili) nikampe shukrani zangu (Bwana wangu)

**kwa kucheza (pia) kwa kuimba (nyimbo) na kuserebuka bila haya (kwani) ninamsifu (mimi) Bwana wangu (Yesu) kwani pekee yeye yuastahili (Yeye) ametenda (sana) mema mengi (kweli) nami sina budi kumshukuru (basi) ndugu zangu (sasa) nawaalika (nyote) tuunganike sote, tumsifu.**

2. Pisha njia niende nikapate uponyaji – all – hebu nipishe upesi niende nikaponywe, Dakitari wangu Yesu sasa ananingoja – hebu …S/A kwani uponyaji (wake Yesu niwa ukweli) aliponya wengi (kwa neno na kwa vazi lake, Nikamwone Mungu mponyaji (wangu) nikampe…..

3. Pisha njia nikimbilie ulinzi kwaYesu – kwani kwake Yesu kuna usalama, Nikiwa naye mashaka dukuduku sina mimi – kwani …. S/A kwake Yesu hamna (mabomu wala vilipuzi) kwake ni amani (umoja furaha upendo) nikamwone Bwana Yesu mlinzi (wangu) nikampe…

Kumalizia:
Sasa shetani ninakutangazia (pisha njia) Unanicheleweshа niondokee, (pisha njia)
Hauna chako nimepata maarifa (pisha njia) Funga virago vyako uende zako (pisha njia)
(ili watu wake Mungu (Baba) wapate nafasi waende kwake Yesu, wakampe utukufu (na nguvu) kwasababu ya ukuu wa jina lake ) x2

Kwa hivyo ondoka SHETANI TOA JAM aee niende nikamwone Masiya
Wakati ni sasa „ „ „ „ „ „ Mwokozi
Mimi si limbukeni „ „ „ „ „ Dakitari
Leo ni mwisho wako „ „ „ „ Yesu.